Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika Allah hadhulumu (hata sawa na) uzito wa chembe; na kama likiwa ni tendo jema, Yeye Atalizidisha na kutoa ujira mkubwa kutoka Kwake.

(An-Nisaa 4:41)

JUZU 79 No. 207 | DH. QA'D - DH. HIJ 1439 AH | AGOSTI 2019 | ZAHOOR 1398 HS | BEI TSH. 500/=

Kiswahili Lugha Rasmi SADC

Na **Pazi Mazongera**

Lugha ya Kiswahili imekuwa ikipiga hatua ya maendeleo ya kutambulika nje ya mipaka ya Afrika Mashariki, pamoja na ukweli kuwa lugha hii imekuwa chachu ya kupigania Uhuru wa Tanganyika. Ni ukweli usio shaka kuwa katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, lugha ya Kiswahili imeimarisha umoja baina ya mataifa hayo. Nchi ya Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo, Burundi, Rwanda, Kenya na Uganda. Watu wanaoishi katika mataifa haya wanafanya biashara na muingiliano wa kijamii kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa kweli ni lazima tukumbuke kwamba lugha hii pia inatambulika kuwa lugha rasmi katika Umoja wa nchi huru za bara la Afrika.

Aidha sikushangaa kuona Marais wa 16 kutoka umoja wa Jumuiya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika wakikubaliana kuwa Kiswahili ni lugha rasmi ya mataifa hayo. Kilichonishangaza ni kushuhudia kasi ya ajabu katika kulienda hilo. Walioneka maraisi wa Afrika ya kusini na



Zimbabwe wakijifunza Kiswahili mapema zaidi ya ilivyotarajiwa na wengi. Rais wa Afrika Kusini Mheshimiwa, Matamela Cyril Ramaphosa ambaye alitembelea mjini Morogoro kwenye kambi ya Mazimbu, yeye alienda mbali zaidi kwani alitoa taarifa ya mtandao (tweet) katika lugha ya Kiswahili.

Katika hili tunampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kwa kuwa kinara katika hili, aliongea Kiswahili fasaha katika mkutano ule na kuwa chachu ya uamuzi huo wa kihistoria.

Kumbukumbu zetu zinasema kuwa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema, Tanganyika haiwezi kuwa huru kama majirani zetu hawako huru. Hivyo Tanzania ikawa kitovu cha harakati za kupigania uhuru wa nchi nyingi za Afrika bilhususi za kusini mwa bara la Afrika. Tanzania ilikuwa ndiyo ilikuwa Makao makuu ya Kamati ya Ukombozi wa nchi za kusini mwa bara la Afrika iliyoongozwa na Marehemu Brigedia Hashim Mbita aliyekuwa mzungumzaji mzuri wa lugha ya Kiswahili.

Uamuzi wa kukifanya Kiswahili kupata heshima hiyo, unanisukuma pia kuwapongeza Watanzania wote na wazungumzaji wa lugha hiyo katika Afrika ya Mashariki, Afrika na duniani kwa ujumla, kwani kutumia kwao Kiswahili ndiyo ukaja msukumo huu na uamuzi huo. Tunabaki na Imani kuwa ipo siku Kiswahili itakuwa pia lugha rasmi ya Umoja wa Mataifa.

Tunawapongeza Marais wetu wa nchi za SADC na kwa kupitia lugha ya Kiswahili umoja wetu utakuwa imara zaidi na hivyo kuleta maendeleo makubwa.

Allah ibariki Tanzania, Afrika Mashariki, Afrika na dunia nzima.

Amin

Mungu Amlilia Machozi Mungu

Na Mwandishi Wetu

Mahubiri yapamba moto usiku na mchana kila kona ya mji wa Dar es salaam. Habari zinazomhusu Yesu wa Nazareti kuhusu uungu wake wa kupewa na wanadamu unafikishwa katika masikio ya watu wote hasa wakilengwa Waislam na wasio na imani za kidini.

KUMRADHI

Katika toleo la mwezi Julai, ukurasa wa 4; tulichapisha tangazo kuhusu Jalsa Salana Tanzania 2019 kuwa itafanyika tarehe 27, 28 na 29 Novemba 2019.

Tunapenda kufafanua kwamba Jalsa Salana Tanzania ya 50 itafanyika tarehe 27, 28 na 29 Septemba 2019.

Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

Pamoja na maneno haya ya Yesu kupewa sifa ya Mungu, kusema kweli Mungu Anachukia sana kuwakasirikia wahubiri wa imani hii ya kishirikina.

Lipo swali linalojitokeza katika vichwa vya watu kuona jambo hili kama halimpendezi Mungu mbona watu hawa wanafanikiwa katika kuwapata watu wanaoamini miongoni mwao wakiwemo Waislamu wenye kujua Mungu ni mmoja?

Watu wanatakiwa kufahamu Mungu siyo kama binadamu mwenye hasira za haraka haraka za kutaka kulipiza kisasi kwa wenye kumchukiza.

Tunasoma Farao zama zake za utawala wake alijipa uungu kule Misri. Watu wake aliokuwa akiwaongoza wenye uelewa mkubwa na wenye uelewa mdogo katika mambo ya dunia, aliweza kuwapumbaza kiasi walimsikiliza kumkubali kuwa ni Mungu wao.

Je Mungu Muumba mbingu na nchi na kila kitu hakumwacha akaendelea na hiyo kufuru yake kwa muda mrefu?

Ili watu hao wasije kuwa na hoja mbele ya Allah siku hiyo ya hukumu, huruma ya Mungu juu ya watu wake aliwatumia mitume Musa (as) na Mtume Haruni (as) kaka yake Musa (as) kwenda kumwonya Farao na wafuasi au raia zake kuwa huyu Farao si Mungu, acheni kumwamini Mungu Amenituma niwaambieni hivyo.

Lakini hebu angalia maneno ya Farao katika mikutano yake ilikuwa ya kumdhalilisha Nabii Musa (as) kwa kumwambia kweli Mungu anawezaje kumtuma mtu mwenye kigugumizi asiyeweza kuongea vizuri? Basi hapo nikuchelewa na Farao kupigiwa makofi. Hivyo ndivyo Mitume na Manabii wote walivyodharauliwa.

Qur'an 36:21 "Ni sikitiko kwa watumishi; hakuwafikia mtume yeyote ila walikuwa wanamfanyia mzaha".

Hapa nakusudia kuwaambia wale watu wanaomkasirikia Mungu wanaendelea kumkasirisha Mungu na mungu aliyezaliwa, aliyehukumiwa mahakamani kwa Pilato, akafa kwa kufika kuzimu ingawa roho mle pangoni haikutengana na mwili, huyo asilani hawezi kuwa ni Mungu. Kufanikiwa kwao kuwapata Waislamu ni wale Waislam jina wasiofahamu dini yao inasema nini kuhusu ni yupi.

Je muda mrefu alioishi Farao katika kufuru yake ya kujipa uungu

Endelea uk. 2

Madhumuni ya Jalsa Salana uk. 10

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kitabu Chekundu

Mara zote Khalfatul Masih V atba amekuwa akisisitiza juu ya kuwepo kwa kitabu chekundu kwa ajili ya Jalsa Salana, siyo tu uongozi wa Jalsa Salana bali pia hata kwa idara zote zilizohusika kwa njia yeyote ile, katika tukio moja alisema:

"mara nyingi, nimekuwa nikisema kuweka kitabu chekundu na kunukuu makossa na mapungufu na kujaribu kuyaondoa. Hii ndiyo njia ya kuweza kuimarisha mfumo wetu. Ni jukumu la Afisa Jalsa salana kufanya vikao na wakuu wote wa idara kila mwisho wa Jalsa. Anapaswa kuwataka walete mapungufu ya idara zao na kuzijadili ili kupata ufumbuzi ili yasijirudie wakati ujao. Mambo yaliyoibuliwa na wahudhuriaji ni lazima yakubaliwe kwa moyo mkunjufu na malalamiko lazima yaondolewe, na mipango madhubuti ya baadaye ifanywe."

(Hotuba ya Ijumaa, 9 Septemba, 2016).

Utamaduni wa kuwa na kitabu chekundu kwa ajili ya Jalsa Salana umeanzia mbali. Ukifuatilia kumbukumbu za Jalsa Salana Rabwah, tumekuta tarehe za nyuma za Jalsa Salana ya mwaka 1954.

Vitu vilirekodiwa kimaandishi, kuanzia kiwango cha vyakula vilivyonunuliwa na kiasi gani kimepikwa kwa kila jiko kwa kila siku. Taarifa za kitabu chekundu ilianza mapema miaka ya 1954, kilianzishwa na Hadhrat Mirza Nasir Ahmad (RA) akiwa ni Afisa Jalsa Salana. Alikuwa akipitia kila ukurasa wa taarifa zilizoingizwa. Kila mwisho wa siku, alimwandikia Hadhrat Khalifatul Masih II (RA) na kutoa uhalisia kwa Huzur aqdas.

Ni jambo la kusisimua kuona taarifa iliyoandikwa na Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (RA) ambaye pia alikuwa ni Mkuu wa wa idara ya kukaribisha wageni. Taarifa ilieleza kwa kina jinsi matatizo yalivyoshughulikiwa na kurekebishwa kutoka mwaka uliopita na marekebisho gani ambayo bado yanatakiwa.

Kinachovutia zaidi ni jinsi kila mmoja alivyotoa mapungufu yote kwa ukweli na uwajibikaji. Ni huu ukweli ndiyo mara zote umekuwa ni alama ya Jamaat Ahmadiyya. Haishangazi kuona Jalsa Salana ikipata mafanikio na maendeleo, kama zilivyo taasisi zingine za Jamaat. Kitabu chekundu lazima kienziwe na kupitiwa kwa ajili ya mipango ya baadaye.

Allah atuwezeshe kufuata kila neno la Khalifatul Masih (atba) kwani, Ni kwa kufuata muongozo wake na kumtii ndiyo tunaweza kuona ustawi na kupata zaidi ya hayo. Insh-a-Allah.

Mungu Amlilia Machozi Mungu

Kutoka uk. 1

utasema alikuwa mkweli?

Tazama mwisho wake baada ya kuonyeshwa miujiza akazidi kuwa mgumu moyo wake, Kutoka 9:35. Kilichofuata ni adhabu ya kuzamishwa katika vilindi vya bahari akazamishwa kama jiwe zito. Hapo mkono mweupe (uwezo) umepata fahari wa uwezo, Kutoka 9:36.

Kusema kweli ndugu zangu kuthubutu bila kuwa na hofu ya kasiriko la Mungu kutangaza kwa kusifu kwamba Yesu ni mungu, kwa kuwa angekuja amevaa uungu wake watu wangeogopa kumsogelea kuongea naye, hizo ndizo hadithi za uongo kama tusomavyo Timotheo 4:3 na 4:4.

Hebu sikieni Mungu alivyomwambia Musa[as] awaambie Waisraeli katika Kumbukumbu la Torati 8:19; "Lakini itakuwa kama ukimsahau Bwana Mungu wako na kuiandama miungu miungine na kuitumikia na kuiabudu, nawashuhudia leo ya kuwa mtaangamia bila shaka."

Ni nani leo atakataa kwamba Yesu na mama yake Mariam amani ya Mungu iwe juu yao hawaabudiwi na kuombwa na sanamu ya Mariam kusimamishwa mbele ya waumini kanisani kwa kusujudiwa waingiapo wakati Mungu Anasema katika Walawi 26:1; "msifanye sanamu yoyote, wala msijisimamishie sanamu ya kuchonga wala mnara, wala msiweke jiwe lolote lililochorwa katika nchi yeni ili kulisujudia, kwa kuwa Mimi ndimi Bwana Mungu wenu."

Hapo hapo unaambiwa katika Walawi 20:8; "Ninyi zishikeni sheria zangu na kuzitenda, Mimi ndimi Mungu niwatakasaye ninyi."

Je ndugu kanisani unakwenda kutubu ili Mungu Akusamehe dhambi zako au unakwenda kuvunja amri na maagizo yake?

Katika lugha ya kimifano unaambiwa kufanya kosa si kosa, lakini jambo baya zaidi ni kurudia kufanya kosa. Wewe unajuwa ni kosa kuabudu sanamu, kulisimamisha mbele yako, kulitumikia, kwa kuliinamia au kulisujudia; kufanya hivyo ndugu yangu ushirikina sawasawa na mvaa hirizi na kutambika.

Isitoshe unaambiwa kuzishika amri ambazo ni maagizo, na unatakiwa kuyatekeleza hayo maagizo ili utakaswe na Mungu. Au wenzetu kuvunja amri za Mungu kwa makusudi baada ya kuelewa unatakiwa ufanye nini kweli? Unatarajia Mungu Akutakase? Tambua anayesamehewa na Mungu ni yule mtu anayekosea au kusahau kwa bahati mbaya.

VIFUNGU VYA MUNGU NI MMOJA

1. Kutoka 20:3 "Usiwe na miungu mingine ila mimi"
2. Kutoka 9:14 "Hapana Mungu mfano wa Mimi ulimwenguni pote"
3. Kutoka 20:23 "Usifanye Mungu mwingine pamoja na Mimi."
4. Kub 6:4 "Eee Israeli Bwana Mungu wetu ndiye Mungu mmoja"
5. Kub 10:17 "Kwa maana Mungu wenu, Yeye ni Mungu wa waungu, Bwana wa mabwana, Mungu wangu Mkuu Mwenye kuogofya Asiyependelea nyuso za watu wala hakubali rushwa.
6. Kub 13:6-8 "Watakapokushawishi kwa siri ndugu yako, mwana wa mamaako au mwana wako au binti yako au mke wa kifuani mwako au rafiki yako aliye kama moyo wako, akikuambia twende (kanisani) tukaabudu miungu mingine usiyoijua wewe wala baba zako, usimkubalie wala kumsikiliza wala jicho lako lisimwonee huruma."

Usiponzeke na ndugu mke na marafiki kuhimizana kwenda kufanya ibada ambayo ndani yake inatajwa miungu kama vile Yesu, Roho na Maria mama wa mungu. Unaambiwa usiwe na huruma ya kusikiliza sauti hiyo ya wito wala usimkubaliye akuitiaye shirki, kama vile huwezi kuwakubalia wazazi wako pindi wanapokuamuru kuabudu mizimu yao ya kijadi. Kama mzazi humtii kwa hilo la kumuasi Mungu, itakuwaje kuwatii viongozi wa kanisa wakati wanakuita katika kukasirikiwa na Mungu kwa kuvunja amri zake?

7. Katika Yohana 15:10 (Yesu) anasema: "kama nilivyoshikia amri za Mungu wangu, Ee ndugu yangu, baba, mama zangu na wajomba zangu ombeni mpate kufunguliwa masikio yenu na macho pamoja na mioyo yenu ili Mungu Awaongozeni kutambua maneno ya uzima ya kumtambua Mungu wa pekee aliye Mmoja hana yeyote mwenye jina hili isipokuwa yeye tu."

Kama Yesu pamoja na utukufu wake hata siku moja hakuweza kuwafundisha watu ya kuwa yeye ni Mungu au roho ni Mungu. Wewe mwenzangu elimu yako si elimu ya ufunuo wa Mungu, ujasiri huo umepata wapi?

8. Isaya 40:18 "Basi mtalinganisha Mungu na nini? Au utamfananisha na mfano wa namna gani?
9. Isaya 42:8 "Mimi ni Mungu ndilo jina langu na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu.
10. Isaya 44:25 "Mimi ni Mungu nifanyaye vitu vyote ni nani aliye pamoja nami?"
11. Zaburi 113:5 "Ni nani mfano wa Mungu wetu aketiye juu?
12. Marko 12:39 "bwana Mungu wetu ni Mungu mmoja.

Naona nimejitahidi kwa msaada wa Mungu kuthibitisha sehemu kadhaa za Biblia zinazoonyesha Mungu ni Mmoja mwenye haki ya kutambuliwa hivyo. Kama mnaona hivyo si kweli, basi onyesheni sehemu yoyote Mungu Alisema Yesu ni Mungu au Yesu mwenyewe katika pita huko na huko kwa mahubiri yake aliwahi kuwaeleza watu yeye ni Mungu. Kama hakuna, na kweli hakuna; basi ogopeni hasira ya Mungu.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Jabali la Mahubiri Limetutoka!

Na Rajabu Abasi Mkieti

Bishara moja ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa ni hii aliyo ahidiwa na Allah kuwa " Nitafikisha ujumbe wako pembe zote za dunia" bishara hii ilibeba hema kuwa Allah atawandaa watu watakao fanya kazi ya kusambaza ujumbe wa nabii. Hii ni moja ya sifa kubwa ya wa Ahmadiyya ambayo alikua nayo Mzee Abasi Mngodo Mkieti.

Je ni nani huyu?

Mwaka 1935 katika kitongoji cha Jibandeni, kijiji cha Lusanga, wilaya ya Muheza, mkoani Tanga. Mzee Ally Salimu Mkieti alibahati kupata mtoto wa kiume ambaye alikuwa wa tatu wa kiume wa Mzee Ally.

Mtoto huyu alipofika makamo Mzee Ally alimpeleka mtoto wake maeneo ya zimbiri Amani kwa mjomba wake Mzee Ally ili asome Qu'rani alikaa huko kwa muda hadi alipofikia muda wa kuanza kusoma shule hapo ndio alirudishwa lusanga kuja kuanza masomo ya shule.

Alianza masomo kijana huyu kwa kupata sifa kubwa kwani alikua akienda umbali mrefu kuifuata shule. Kijana huyu alikuwa na mapenzi makubwa na dini tukufu ya Islam kwani akiwa darasa la tatu aliomba ruhusu kwa Mwalimu mkuu ya kwenda kusali sala ya Ijumaa alikubaliwa kwa muda fulani. Ruhusa hiyo iliwashawishi wanafunzi wengine kuomba ruhusa. Hapo ndipo mwalimu wake alipoona ni muhimu kuhakiki je ni kweli wanafunzi hao wa Kiislamu wanaenda kweli msikitini siku hiyo ya Ijumaa baada ya muda Mwalimu Herbert aligundua kuwa katika wanafunzi wote ni mwanafunzi mmoja tu ambaye ni Abasi ndiye anayeenda msikitini kwa ajili ya Ijumaa wengine walitumia fursa hiyo kwenda mitaani kucheza. Hapo Mwalimu Herbert aliwaita wanafunzi wote wa shule yake na kuwatangazia kuwa kuanzia leo mwanafunzi pekee atakayeruhusiwa kwenda msikitini ni Abasi Mngodo Mkieti siku ya Ijumaa tena itakapo fika muda wa sala yeye ataondoka bila ya kuomba ruhusa. Hapo Alianza kupata umaarufu mkubwa kwani baba yake alikua ni mwakilishi wa kiongozi wa kimila wa serikali ya Kikoloni ambaye ni Ashirafu Mwaimu-Jumbe mkuu katika kijiji chao.

Mapenzi ya Mzee Ally na kijana wake yalizidi kuongezeka kwani kijana huyu alikua na adabu kwa watu wengi. Ilipo fika 1952 mwaka huo ndio ilikua mwaka wa huzuni wa kijana huyu Abasi Mkieti kwani baba kipenzi Mzee Ally aliaga dunia. Hapo kijana huyu alikua ameanza kusoma darasa la tano hapo alishindwa kuendelea na masomo kwani hakukuwa na mtu wa kumlipia ada.



Marehemu Abasi Mngodo Mkieti (wa kwanza kushoto) akiwa katika banda la Mapenzi ya Mungu katika Jalsa Salana Tanzania 2018. Wa kwanza kulia ni kijana wake, mwandishi wa wasifu huu.

Akaanza kutafuta shughuli za kumpatia kipato katika Maisha. Hapo ilimlazimu aende Korogwe kufundishwa ufundi wa viatu kwa Wahindi ambao walikua ni maarufu kwa ufundi wa viatu. Kiujumla alipata kuona maisha ya jamii hiyo ya Wahindi ambao walifanya ibada ndani katika nyumba zao. Kwani alikuwa na ukaribu kiasi cha kuaminiwa na kupewa majukumu ya kuagizwa hapa na pale. Akiwa bado ni mwanafunzi kwa fundi wake huyo alipangiwa kazi ya kumpeleka mbwa wa mwalimu wake mtoni yeye na wanafuzi wenzake hapo kwa mwalimu wao, jambo hilo wanafuzi wenzake halikuwafurahisha hadi kupelekea wanafuzi wenzake kugoma kumpeleka mbwa huyo mtoni. Yeye alilifanya tena kwa furaha. Akiwa hapo kwa mwalimu huyo wa Kihindi jamii ya Masingasinga aliona maisha yao juu ya imani na wanavyoamini juu ya Mungu daima katika maisha hayo yeye alikuwa akitafakari juu ya ipi ni dini ya kweli, na ni ipi dini itokayo kwa Mungu, na ipi dini itokayo mfikishe mja kwa Mola wake.

Alimaliza mafunzo kwa fundi wake. Sasa ni fundi alijipanga kuhama kutoka Korogwe kuja Tanga mjini. Alipohamia Tanga mjini mwaka 1957 hapo akafungua ofisi yake ambayo ilikua barabara 15 masikini ya bomboka.

AANZA KUTAFUTA DINI YA KWELI.

Akiwa hapo Tanga mjini alipata jazba zaidi ya kufanya uchunguzi wa dini ili dini atakayoiona ya kweli ajiunge nayo. Kwanza alianza na dini ya Masingasinga ambayo fundi wake alikuwa anaiamini hapo alipofika katika nyumba za ibada za Masingasinga.

Haikua rahisi kupata mwalimu kwani kulikua na vikwazo vingi hali hilo ili mlazimu kuhamia dini ya Ukristo

Katika dini ya Ukristo alipata hamasa kubwa kwani katika kila kanisa na makundi aliko pita ya kikristo alipewa fursa ya kusoma imani ya kila kundi kwa undani na nini hasa kitu kinacho itwa dini. Wakati huo akifanya uchunguzi alikua ni Mwislamu lakini katika dini hiyo hakuwa na elimu yoyote ambayo ni rahisi unaweza kupitia kwani hata kitabu ambacho ndio muongozo wa dini ya kiislamu kilikua ni Kiarabu kwani ni watu wa chache sana walikua wana kielewa.

Katika kila kanisa alipatiwa mwalimu na alipangiwa muda wa kuja kusoma. Kila alipomaliza masomo aliombwa kusoma na lingine. Yeye muda wote somo kubwa alililiomba kusoma hasa. Dini ni nini na na dini gani ya kweli katika dini zote zilizopo duniani.

Katika hali hiyo ya kutafuta ukweli wa dini na kumtafuta Mungu aliweza kupata marafiki wengi akiwamo "father" Odilo, "sister" Scolast Msofi na wengine wengi.

Baadaye aliamua kuelekea katika dini Tukufu ya Islamu. Hapo ndipo alipokuta katika Uislamu hakuwa na chochote usipo kuwa ni jina tu katika msikitini ulio Karibu na Garden ya uhuru hapa Tanga palikuwa na sheikh mkubwa alimwendea akamuomba ili apate kujifunza dini lakini alikatishwa tamaa kwa maneno ya Shekh kuwa umri wake kuwa mkubwa na haijui dini yake. Baada ya kuzunguka katika misikiti na madrasa kadhaa za kitovu kikubwa cha elimu ya dini ya Kiislamu Tanga bila mafanikio alirudi kuendelea na mafunzo yake katika makanisa mawili Roma na Angalikani ambayo yameshika mizizi sana kati mkoa huu wa Tanga kipindi hicho.

Katika nyumba ambayo alikua anafanyia kazi kulikua na nyumba ya jirani ambayo ulikua zamani ni madrasa Mwalimu huyo mwenye hicho chuo alikua ni muislamu lakini msuni yeye alijiungu na jumuiya pamoja na wanafunzi wake wa tano Mzee huyo alikua mchamungu. Baada ya kujiunga na Jumuiya mji mzima wa Tanga ulijua kuwa Sheikh huyo amerogwa na makadiani. Mzee huyu alivutiwa na kijana huyu Abasi Mkieti ambaye muda wote anajishughulisha na kutafuta dini ya kweli. Hali hii ilimsogeza Karibu na kuanza kumhubiri. Kijana huyu alimueleza kuwa mimi natafuta dini ya kweli je katika jumuiya yenu naweza kupata mwalimu wa kunifundisha dini, na uwepo wa Mwenyezi Mungu. Alimjibu ndio. Siku ikapangwa ya yeye kukutanishwa na mwanachuoni mkubwa Maulana Sheikh Abuutwalibu Sandi. Mzee Hasani akiwa na kijana huyu waliingia katika msikitini wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanga Masjid Ihsan. Walimkuta mapema Sheikh Abuu Twalibu anamsubiri mwanafunzi. Kama ujuavyo MaSheikh wa Jumuiya ya Ahmadiyya hawana maringo wala majivuno, kazi yao ni kufundisha. Mzee Hasani alimueleza dhumuni la bwana Abasi Mkieti kuwa yeye amekuja kujifunza tu juu ya dini ni nini na ni ipi dini ya kweli kama ataridhwishwa atajiunga nayo.

Maulana Sheikh Abuu Twalibu Sandi hakufanya ajizi yeye akampangia Mwanafunzi huyo kila siku baada ya sala ya magharibi darasa lao litaanza. Mwanafunzi alifurahi kuona kuwa katika dini ya Islam aliyozaliwa amepata

Endelea uk. 8

Mfumo wa Ndoa Katika Islam

Imefasiriwa na Abdulkarim Yusuph

Ukiangaliakwaundanimafundisho ya dini tukufu ya Islam, utagundua uzuri wa mafundisho ya dini hii, na hii hutupatia kwa ukamilifu wa mambo yote ya maisha ya mwanadamu. Utaona ya kuwa maelezo yanayohusu ndoa yapo kamili kote katika Qur'an tukufu na Hadith (mafundisho ya Mtume Muhammad, Rehema na Amani ziwe juu yake). Mfumo wa ndoa ni kitengo cha msingi cha jamii ya mwanadamu na kimetengeneza msingi wa familia. Familia zenye afya zinatakiwa kushikamana na kuzitunza familia zao dhidi ya harakati zingine za mwanadam.

Kwa hiyo Allah huwaamrisha waaminio kuoa kwa faida za kimaadili, kiroho, kijamii na kisaikolojia.

Mtume Muhammad*saw* alisema

"ndoa ni amri yangu na mafundisho yangu. Watu ambao hawafuati mafundisho yangu sio katika waumini wangu"

"pindi mwanaume anapooa, anakua amekamilisha nusu ya dini yake"

Khalifa wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa*as* ameelezea jukumu la ndoa katika kukamilisha mafundisho kwa ndugu zetu ambayo ni baada ya mahusiano yetu na Allah. Anatuhimiza

"ni jukumu letu kuona ya kuwa ni lazima kuheshimu na kuzingatia juu ya imani. Ndoa inahusu jukumu kubwa sana kwa mwanaume na mwanamke, lakini nimeweza kuona watu wachache wametambua hili. Pindi wanapo oa, hulifanya katika kiwango kidogo sana. Sheria za Islam zimeweza kututofautishia katika vipengele viwili.

Cha kwanza ni kujihusisha binafsi na Allah na cha pili ni kujihusisha na wenzetu pia (mwanadamu). Ndoa imeweza kuingia katika kipengele cha pili na kinaweza kuangaliwa kama kipengele tetezi. Sheria za Islam zimeweza kuelezea zaidi juu ya hili, lakini kuna watu wengi ambao wanaonekana kutoelewa (sheria) vizuri. Labda wanajaribu kujibinafsisha wenyewe na jambo hili. Mada zao ni kama mtoto ambae anaweza kuwa kimya akiwa na uhitaji wa almasi nzuri kwa ajili ya msingi wa sarafu.

Unaweza kuona, ndoa ni kitu muhimu sana kwa muIslam. Lakini utaweza kugundua yote hayo kama utajizatiti kiroho na kimwili na kama utaweza kutimiza maagizo na maelekezo kutoka kwa Allah na Mtume wake (rehema na amani za Allah ziwe juu yake) juu ya mahusiano na familia. Kuanzia katika uchaguzi mzuri wa mwenza mpaka katika masuala ya familia.

Unaweza kuona ya kuwa mpangilio mzuri, wajibu mzuri, kazi na mpangilio wa mafanikio; ambayo yote hayo yanaleta usalama kwa wote ndani ya familia. Kwa ujumla



Islam inatufundisha na kutujulisha wajibu wa kila mtu katika familia.

KUSUDI LA NDOA KATIKA ISLAM

Allah kaleta ndoa kwa waaminio kwa misingi mikuu mitatu. Nayo ni

1. Kumuwezesha mwanaume na mwanamke kuishi pamoja na kuonesha upendo na furaha, bila kuvuka mipaka ya Islam.
2. Kupata watoto na kupata msingi mzuri wa dini kwa ajili ya ukuaji wao
3. Kupata umoja uliokua wa halali ambao unalinda matakwa ya jamii kimaadili na mchanganyiko wa jamii husika.

Makusudio ya kwanza yote yanajieleza yenyewe; yote yanaelezea asili ya mwanadamu. Kusudi la tatu linamuangalia zaidi mtu mmoja mmoja, na hutambulisha ndoa kama jambo muhimu katika ujengaji wa jamii.je ndoa inakamilisha jambo hili?.

Cha kwanza tunachotakiwa kujua ni jambo ambalo ni muhimu, tabia nzuri ndani ya Islam ni usafi; ya kwamba, usafi ambao ni wa wote yaani ni wa binafsi au jamii nzima. Islam inatambua ndoa kama ni jambo ambalo mwanadam hukamilisha mahitaji yake. Yote ya kimwili na kihisia, yote hayo hudhibitiwa na kukamilishwa katika wakati mmoja. Jambo ambalo si halali na lisilodhibitiwa ambalo hutaka kufurahisha matakwa binafsi nje ya ndoa hayo hayaruhusiwi ndani ya dini tukufu ya Islam. Zinaa na uzinzi ni dhambi zilizokatazwa kabisa. Mwanaume muislam haruhusiwi kwenda kwa mwanamke yoyote na kujirdhisha matakwa yake ya kimwili na matamanio. Anatakiwa atimize na atekeleze mkataba halali wa ndoa, ambao unatimiza uwajibikaji wa ziada,wajibu na majukumu ya familia na watoto kwa maisha yake yote atatimiza.

Matokeo ya mipaka hii ni uundaji wa jamii ambayo kwayo tabia njema zinalindwa. Hii ni kusema ya kwamba, Qur'an tukufu imetaja mkataba wa ndoa (nikah) kwa neno la ihsan, ambalo linamaanisha ngome. Mwanaume ambaye ameoa huitwa ***muhsin***, ambayo yamaanisha aliyejenga ngome. Mwanamke ambaye ameolewa na mwanaume huyo huitwa ***muhsinah***, ambalo linamaanisha kuwa yeye amekuja ndani ya ulinzi wa ngome hiyo, kwa nia ya kujilinda mwenyewe na maadili yao.

NAMNA YA KUISHI KABLA YA NDOA

Ni lazima ieleweke vizuri kuwa Islam hairuhusu mahusiano ya jinsia mbili, hata mahusiano ya mapenzi ya kimwili, nje ya ndoa. Kukaa mbali na vitendo vya mapenzi na kuviepuka kabla ya ndoa ni jambo la muhimu sana lililoelezewa ndani ya Qur'an tukufu.

Zinaa na uzinzi na kuwa na mahusiano ya kujificha katika jinsia mbili tofauti ni tabia mbaya na isiyofaa ambayo imekatazwa vikali sana na dini tukufu ya Islam. Makatazo haya yanahusisha

Uchumba, kuwa na hawala ambao wanaishi pamoja. Yote hayo yanachukuliwa kuwa ni dhambi kubwa, ambazo zinabeba adhabu kubwa sana. Kama isemavyo Qur'an tukufu sura ya 24:3-4

3. ""Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, basi mpigeni kila mmoja wao mijeledi mia. Wala isiwashikeni kwa ajili yao huruma katika hukumu ya Allah, ikiwa ninyi mnamwamini Allah na siku ya Mwisho; na lishuhudie adhabu yao kundi la waaminio".
4. "Mwanamume mzinifu hafungamani ila na mwanamke mzinifu au mwanamke mshiriki; na mwanamke mzinifu hafungamani naye ila mwanamume mzinifu au mshiriki; na hayo yameharamishwa kwa waaminio"".

Qur'an tukufu imeelezea vizuri ili kuweza kudumisha usafi. Inatuongoza mwanaume na mwanamke katika kujizuia kuangaliana baina yao kwa uwazi sana jambo ambalo linaweza kuleta matamanio juu yao. Inatuongoza kwa undani zaidi kwa wao kujizuia masikio yao katika kusikia maongezi ya majaribio na matamanio,na kujizuia na hafla ambazo zinaweza kuwapelekea katika majaribu. Kufunga sunna, kula mlo kamili na mazoezi yanasaidia kujidhibiti na matamanio na kudumisha usafi wa roho.

UCHAGUAJI WENZA

Jambo ambalo ni zuri katika kujenga ndoa imara ni katika uchaguaji wa mtu ambaye utakaa naye katika maisha yako yote. Hapa tena, Islam imeweza kutuongoza.

Mtume Muhammad*saw* alisema

"Mwanamke anaolewa kwa sababu nne mali yake, ukoo wake, uzuri wake, na dini yake. Basi upate ufaulu kwa kujichagulia mwanamke mwenye dini".

Uzuri au maadili mazuri ni jambo zuri sana la kuangaliwa katika uchaguaji wa mwenza. Kama mtu na mwenza wake wana ukweli na uaminifu ndani yao wataweza kuyafikia matakwa yote ya ndoa katika njia za kumuogopa Allah na watajaribu kuweka mambo katika ufaulu. Kitu kingine ambacho kinatakiwa kuangaliwa katika uchaguaji wenza ni ukoo wa mwenza, umri, na elimu. Sala ni jambo la muhimu sana katika uchaguaji wa mwenza. Waislam tumefundishwa sala ya istikhara kwa ajili ya kupata muongozo wa Allah katika kufanya uchaguzi bora wa mwenza.

Kukiwa na fikra hizi kichwani, ndoa kwa waIslam inapangwa na watu wote wawili mwanaume pamoja na mwanamke. Wazazi au walezi huandaa ndoa kwa watoto wao pindi wanapofikia katika umri sahihi na upeo wa ukuaji ukiwa sahihi. Kama umeweza kuishi katika jamii za kimagharibi unaweza kuona jambo hili kuwa ni gumu sana lakini limeweza kutekelezwa kwa kipindi kirefu sana na linatoa familia imara na zenye furaha. Ulinganishaji wa talaka zinazotolewa miongoni mwa jamii za magharibi ni chache, ndoa hudumu na zinalindwa zaidi kwa muda mrefu.

Ukweli katika jambo hili ni kwamba wazazi au walezi huwa wanajua tabia za watoto wao vizuri, na hujaribu kuchagua mwenza ambaye anaweza kuendana vizuri na mwenziye. Pindi mwanaume na mwanamke wanapokuwa na uchumba kuna hatari kuwa matamanio yanaweza kuzidi matakwa yao. Wanaweza kuwa na matamanio ya nafsi

Inaendelea uk. 5

Mfumo wa Ndoa Katika Islam

Kutoka uk. 4

pekee, lakini wanapoingia katika ndoa na hukuta mapungufu ya kila mtu pindi wanapokuwa wamechelewa sana. Matamanio ya nafsi au ya kimaumbile, au "kuwa katika mapenzi" yanaweza kusababisha matatizo mengine hapo mbele ambayo yanaweza yakapelekea kutokuwa na hamu ya ndoa hiyo hapo baadaye, ambayo yatapelekea mvunjiko wa ndoa. Katika maono mengine ndoa ambayo imepangiliwa, muonekano wa kimaumbile huchukua nafasi ndogo sana na wahusika wa ndoa hiyo hawaingii katika ndoa hiyo wakiwaza kupata mapenzi ya kimaumbile tu, lakini huona kama ndoa ni maisha ya umoja ambayo humhitaji kila mtu kujitoa na kuwa na roho ya kumsaidia mwenza wake. Ujengaji mzuri wa heshima, uaminifu yote hayo hutengeneza daraja baina ya mume na mke ambalo ni imara na huwa na uhimili zaidi kulikoni ndoa ambazo hufungwa kwa matamanio ya nafsi au ya mwili tu.

Hakuna ndoa inaweza kuandaliwa na kufungwa bila idhini ya mwanaume na mwanamke. Japokuwa mwanamke huhitaji mlezi au mwakilishi kwa ajili ya uandaaji wa ndoa hiyo. Dhumuni kuu la mwanamke kuwa na mwangalizi ni kulinda haki zake na kuongea na kila mtu kabla ya ndoa, akiwa kama walii katika maongezi hayo.

Kama mwanamke ameweza kuikubali Islam na wazazi wake si waislam, anaweza kumteua mtu yeye mwenyewe kama atahitaji kuolewa. Hii inaweza kufanikiwa kwa kumuomba mtu mmoja yeye mwenyewe kwa chaguo lake mwenyewe, au kuomba Jamaat katika idara husika kumchagulia mtu mmojawapo. Mwangalizi ambaye anatakiwa kuwa mwanaume, ana jukumu la kulinda sheria, za kidini, kijamii, haki zote za ndoa na mahari, kama kitu chochote kitahitajika mlezi huyo anatakiwa kuandaa kitu hicho.

Idara ya ndoa katika Ahmadiyya ina mfumo wa taarifa unaostahiki kwa wanaume na wanawake. Taarifa zinapatikana kwa muahmadiyya mzuri ambaye atastahiki katika sifa zote ikiwemo umri n.k jambo ambalo litakua na faida kwa mwanamke. Kama atakua anahitaji anaweza kuuliza kwa Raisi wa tawi jinsi ya kufanya ndoa sahihi kwa mfumo huo wa taarifa za idara ya ndoa. Lakini taarifa hizo zote ni za siri kabisa.

MAKATAZO KUHUSIANA NA NDOA

Allah ameweza kutuwekea mambo ambayo yamekatazwa kuhusiana na ndoa, na mambo mengine ya mahusiano baina ya mwanamke na mwanaume.

1. Kuna watu ambao muislam haruhusiwi kuwaoa kama isemavyo Qur'an tukufu sura ya 4:24

"mmeharamishiwa kuoa mama zenu, binti zenu na dada zenu, na shangazi zenu, na dada za mama zenu waliowanyonyesheni, na dada zenu wa kunyonya, na mama za wake zenu, na binti zenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia- lakini kama nyinyi hamjawaingilia, basi si vibaya kwenu (kuwaoa) – na wake wa wana wenu waliotoka katika migongo yenu; na (imeharamishwa) ya kwamba muwaoe madada wawili wakati mmoja, isipokuwa yale yaliyokwisha pita; hakika Allah ndiye msamehevu, mrehemevu."

Lakini pia MuIslam anaruhusiwa kumuoa binamu yake.

2. pia dini tukufu ya Islam imeweka wazi kuhusu ni akina nani wanaoruhusiwa kuolewa kama yeye dini yake yahusika. Ndoa na muabudu masanamu hiyo imekatazwa na dini tukufu ya kiIslam. Kama isemavyo Qur'an tukufu sura ya 2:222

"wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini. Na bila shaka mjakazi mwenye kuamini ni bora kuliko mwanamke mshirikina ingawa awapendezani. Na wala msiwaoze wanaume washirikina mpaka waamini. Na kwa yakini mtumwa mwenye kuamini ni bora kuliko mwanaume mshirikina ingawa awapendezani; hao wanaita kwenye moto, na Allah huita kwenye pepo na samahani kwa amri yake. Naye hueleza aya zake kwa watu ili wapate kukumbuka."

Zaidi inatakiwa ijulikane ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa[as] ameweka ukomo kwa "watu wa kitabu" Wayahudi na Wakristo. Pia amekataza waahmadiyya wanawake katika kuolewa na wanaume wasiokuwa waahmadiyya. Sababu katika jambo hili ni kwamba, mwanamke haruhusiwi kuolewa nje ya imani yake, kwa sababu pindi anapokuwa katika nyumba ya mumewe na mazingira yao yeye pamoja na watoto wake hushirikiana na watu wasiokuwa waislam na waahmadiyya. Hili huleta ugumu kwa yeye kuendelea kuwa imara na imani yake na kuwalea na kuwakuza wanaye kama waislam. Mwanaume anaweza akamshawishi mkewe na kumleta ndani ya njia na sheria za Kiislam.

SHEREHE YA NDOA YA KIISLAM

Kuna vitu vinahitajika kwa ajili ya ndoa kuwa halali:

- Wote mwanaume na mwanamke lazima wakubali kwa hiari yao ndoa hiyo, kabla haijafanyika.
- Ndoa inatakiwa ifanyike hadharani, kwa kuwa na mashahidi wawili kutoka pande zote mbili waliokuwepo katika sherehe hiyo. Islam hairuhusu ndoa za siri.
- Bwana harusi na walii wanatakiwa wawepo katika nikah. Bwana harusi anaweza au asiweze kuwepo.
- Mahari ni zawadi ya lazima kutoka kwa mume kwenda kwa mke. Kama isemavyo Qur'an sura ya 4:25

" .....Na mmehalalishiwa (kuoa wanawake) minghairi ya hao. Kwamba muwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila kufanya zinaa, na kwa ajili ya faida mnayoipata kwao, basi wapeni mahari zao zilizolazimishwa; wala si vibaya kwenu katika yale mliyoridhiana baada ya mahari. Hakika Allah ni mjuzi, Mwenye hekima."

Mahari hutangazwa katika hafla ya ndoa. Inaweza kutolewa yote kwa pamoja au katika utoaji wa makubaliano. Pindi inapotolewa ni mali ya mke na anaruhusiwa kuitendea atakacho kwa idhini yake yeye. Kiasi kinatakiwa kikubaliwe katika pande zote mbili.

Ndoa haswa hufanywa kwa mamlaka halali ya Islam, yaweza kuwa mbashiri au rais wa jamaat. Taratibu za ndoa hiyo ni rahisi. Pindi fomu za ndoa zinapojazwa na ndoa imetangazwa hadharani na mashahidi wakashudia, mkataba wa ndoa ni halali. Mfungishaji ndoa husoma sura ambazo Mtume Muhammad[saw] alizisoma na kuuliza idhini kwa pande zote mbili. Baada ya hapo hufuatia maombi.

Wanandoa huhitajika kupata cheti maalum cha ndoa na kitu chochote kinachohitajika na nchi hiyo. Baadhi ya nchi za ulaya mtu ambaye anaoa anatakiwa awe raia kamili wa nchi hiyo.akiwa amekidhi vigezo vyote vya uraia anaruhusiwa kufunga ndoa. Kama anakua hajakidhi vigezo kamili vya nchi hiyo inabidi atangulize sherehe yao ya dini na sherehe za kiraia, ambazo zinazofanyika katika ukumbi wa jiji. Waangalizi wa bi harusi wanatakiwa kuzijua hatua zote hizo ili kuhakikisha ya kwamba haki za bi harusi kama mke ni halali na zinazingatiwa.

Sunnah za Mtume Muhammad (rehema na amani za Allah ziwe juu yake) alikua akifanya walimah, ambao ulikua ukifanywa na bwana harusi baada ya ndoa kwa ajili ya kusherehekea kutimiza kufunga ndoa hiyo. Hii ni sehemu ya muhimu katika sherehe za ndoa na inatakiwa iwe kwenye utaratibu katika mipangilio ya mume. Khalifa wetu wa zama ametambua kuwepo kwa ukarimu lakini ametutahadharisha Waislam juu ya ubadhirifu katika sherehe za ndoa.

Itaendelea toleo lijalo

Ifuatayo ni orodha ya **Kamati Kuu ya Uongozi** wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia **Julai 2019** hadi **Juni 2022**, kama ilivyoidhinishwa na Hadhrat Khalifatul Masih V[atba]

Na.	Jina	Nafasi
1	Tahir Mahmood Chaudhry	Amir na Mbashiri Mkuu
2	Bakri Abedi Kaluta	Naibu Amir - Tabligh na Tarbiyyat
3	Issa Mwakitalima	Naib Amir - Fedha
4	Seif Hassan Nakuchima	Katibu Mkuu
5	Abdulrahman Mohammed Ame	Katibu Mkuu wa Ziada
6	Ali Khamis Mbambwa	Katibu wa Tabligh
7	Ramadhan Hassan Nauja	Katibu wa Tarbiyyat
8	Abdallah Jaffar Msesemele	Katibu wa Dhiafat
9	Said Salum Mgeleka	Katibu wa Taalim
10	Dr. Swalehe Kitabu Pazi	Katibu wa Ishaat
11	Karim Mohammed Mpate	Katibu wa Waqf Jadid
12	Muharram Juma Kawambwa	Katibu wa Samiu Basir
13	Rajab Abbas Mkieti	Katibu wa Tahrik Jadid
14	Ramadhani Hassan Mrope	Katibu wa Fedha
15	Omari Ali Mnungu	Katibu wa Ziada wa Fedha
16	Amir Abedi Kaluta	Katibu wa Waqf Nao
17	Inayatullah Seif Nakuchima	Katibu wa Rishta Nata
18	Jamhuri Kahewanga	Katibu wa Ziraat
19	Rahim Iddi Mwanga	Katibu wa Umur Khaarijah
20	Mussa Salum Mgeleka	Katibu wa Jaidad
21	Abdulaziz Kitabu Pazi	Katibu wa Sanao -Tijara
22	Mwinyimvua Mohammed Ussi	Katibu wa Umur Amma
23	Munawwar Athumani Mkoka	Katibu wa Tajneed
24	Mohammed Mwinyimvua Ussi	Katibu wa Wasia

Bustani ya Washairi

SALAM

1. Salamu na wasalimu, funguo ya muungwana,
Natoa kwa tabasamu, hata tusipojuana,
Tutoleane salamu, kisha ndo kuulizana,
Salamu kutoleana, ndo utu wa mwanadamu.

2. Hakuna mwenye salamu, uwe mzee kijana,
Wote inawalazimu, pindi mnapokutana,
Mwenye cheo kwa Karimu, Yule wa kwanza kunena,
Salamu kutoleana, ndo utu wa mwanadamu.

3. Wapo wanaodhulumu, wanaringa kujiona,
Hawaoni umuhimu, wa hali kujuliana,
Kazi yao kulaumu, kwa kujiona mabwana,
Salamu kutoleana, ndo utu wa mwanadamu.

4. Na wengine wahujumu, wakubwa hata vijana,
Salamu kwao ni sumu, vibaya kuaziana,
Hawajui ni karamu, binadamu kupendana,
Salamu kutoleana, ndo utu wa mwanadamu.

5. Na mwenzenu sina hamu, yaliyonikuta jana,
Kaja bwana wa makamu, nimuazime amana,
Kaomba bila salamu, haraka nipe kijana,
Salamu kutoleana, ndo utu wa mwanadamu.

6. Kweli salamu ni tamu, yaondoa kujivuna,
Katu usiweke zamu, thawabu utazivuna,
Uchunge yake nidhamu, upitapo kila kona,
Salamu kutoleana, ndo utu wa mwanadamu.

7. Amkizi la kudumu, ametupa Maulana,
Salamu alaikumu, toa bila kunong'ona,
Hiyo ni njema salamu, itika sio kununa,
Salamu kutoleana, ndo utu wa mwanadamu.

8. Naweka chini kalamu, hapa mwisho wa kunena,
Mola wetu Muadhamu, tupe macho ya kuona,
Tuidumishe salamu, e Mola wetu Rabbana,
Salamu_kutoleana, ndo utu wa mwanadamu.

MWL. NAJAT FAKIM SAID NANG' OLO
(THE BIG BOSS)
MAGOZI JUMAAT-IRINGA

VITABU VYAKE MASIHI

1. Mungu nipe fahamu, Beti hizi kutimiza,
Hakika ninayo hamu, Masihi kumpongeza,
Kuhimiza majukumu, Ya dini kuieneza,
Vitabu vyake Masihi, Funuo za kimbingu.

2. Vinavyo nyingi elimu, Ya kuhuwisha imani,
Funuo hizi muhimu, Za vitabu themanini,
Mungu kampa elimu, Ya dunia na kidini,
Vitabu vyake Masihi, Funuo za kimbingu.

3. Alishikishwa kalamu, Na muumba wa mbinguni,
Kwa malengo maalumu, Kuimarisha imani,
Kateuliwa hakimu, Kusimamisha yakini,
Vitabu vyake Masihi, Funuo za kimbingu.

4. Elimu yake i ndani, Vya kusoma umakini,
Tuimarike kiimani, Kwa elimu ya mbinguni,
Sote tuwe waumini, Wa kushika uchamungu,
Vitabu vyake Masihi, Funuo za kimbingu.

5. Mtume alitabiri, Kufika kwake Masihi,
Kurani kuifasiri, Kwa sifa ya umasihi,
Qur'ani kukariri, Elimu ipo kichwani,
Vitabu vyake Masihi, Funuo za kimbingu.

6. Hekima ya Isilamu, Kitabu chake Masihi,
Kitabu hiki malum, Kujibu hoja sahihi,
Kutetea Islamu, Ndiyo dini ya kwelii,
Vitabu vyake Masihi, Funuo za mbinguni.

Madumla Ng'amilo

NDOA

1. Ndoa ni liwaza njema, tena ni kitu murua
Ukitaka mke mwema, jitahidi nyingi dua
Kuoa jambo lazima, kwa mtu aliyekua
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

2. Oa unayempenda, katika kabila zote
Hata Ikwiriri nenda, Madangwa au Makete
Ukioa tajilinda, ukapera hali tete
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

3. Nikah sio utani, au mtu chalechale
Ndoa ni kitu fulani, iliyo baraka tele
Lianza toka zamani, wakati wa enzi zile
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

4. Ndoa ni maelewano, baina ya wanandoa
Wala sio mapigano, mpaka jino kung'oa
Yahitaji mapatano, ugomvi ukitokea
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

5. Nikah ni maamuzi, kwa wote wapendanao
Wala sio uchaguzi, wa kugombania vyeo
Tena si ligi la mbuzi, kutoana hadi ngeu
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

6. Ndoa kwa watu sitara, machafu huyaondoa
Usihofu ufukara, kijana ushindwe oa
Bila ya ndoa madhara, uchamungu wapotea
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

7. Nikah tusiibeze, vijana tubadilike
Zinaa tusiikweze, kuoa tuwajibike
Kwenye ndoa tusicheze, nikah iheshimike
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

8. Ndoa nayo ni ibada, yenye uchamungu nusu
Pia pepo ya ziada, Mwenyezi Kairuhusu
Kuoa kuna faida, wala sio mahabusu
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

9. Kuoa unajilinda, na maradhi ya dunia
Wenye ndoa wameshinda, kwa Mungu waheshimiwa
Vijana funga mkanda, fungeni hadi na ndoa
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

10. Vijana msiwe bize, na mapambo ya dunia
Ni bora niwaeleze, msije mkajutia
Kuoa msikawize, maovu mtaingia
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

11. Ndoa yataka subira, upendo mwingi nidhamu
Sio kukunjiana sura, wala sio uhasimu
Ndoa mfano shajara, wenye tunda tamutamu
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

12. Vijana sibabaike, na mambo ya ujanani
Sasa hivi oa mke, sisubiri Ramadhani
Ili futari apike, mwezi kisha toka ndani
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

13. Wanaume nawaasa, sikilizeni vizuri
Kuoa kuachaacha, sio tabia nzuri
Wadaiwa wanenepa, jua sifa ya kiburi
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

14. Ndoa ni kama amana, Mwenyezi Ametugea
Wanandoa mche Rabana, imani mtolegea
Kuswali swalini sana, funga iwe mazoea
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

15. Bado bado najipanga, ndicho kigezo cha wao
Ndoa wataki kufunga, mpaka wawe na vyao
Ila wa mbele washenga, kwa sherehe za wenzao
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

16. Ndoa yataka utii, nalo hilo mfahamu
Mume kwako hutulii, kama yu nesi wa zamu
Mke wampa bipii, yuko wapi baba Mamu
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

17. Michepuko si mizuri, Rahimu Amekataza
Nikah imekusitiri, vipi wa nje kuwaza
Bora uoe wa pili, kama huwezi jikaza
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

18. Maneno maneno mengi, wanawake punguzeni
Mume akikosa chenji, bora muvumilieni
Simuone ye mshenzi, riziki ni ya Manani
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

19. Ndoa ndoa ndio neno, ambalo namalizia
Ndoa wala si ndoano, ni jambo la nadharia
Ndoa nayo mapatano, kwa mujibu wa sheria
Kuoa ustaarabu, wa maisha ya dunia

Ahmad Msham Namwadila (Ahms Law)

ISHI KWA UNYENYEKEVU

Jina lako litukufu, siioni mithilie.
Nikuanzie raufu, barakazo nitilie.
Napindama mdhaifu, wewe ni kusudie.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Takabuli tahadhari, kwa unyenyekevu ishi.
Usijitie fahari, kuendekeza ubishi.
Kujiona u hodari, mbora wa matamshi.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Ati mimi ndo shupavu, ngangari kama mlima.
Wengine wote wachovu, nini kwangu watasema.
Unakosa usikivu,busara zake mnyama.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Mfa maji baharini, mzamivu maridadi.
Agongae baharini, dereva mwenye weledi.
We ni nani jamani, kujikweza kweza hadi.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Mwishoe unairuka, mipaka yake karimu.
Unaanza ushirika, unaacha isilamu.
Waona melimika, kumbe hauna elimu.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Kwamba wewe ndo tajiri, hakuna mtu afike.
Unajawa ujahiri, tangu pesa uzishike.
Ingawa kuna fahari, ni vipi asisikike.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Hadi kwenye uchamungu, wajiona mtimivu.
Unawapiga majungu, wengine ni wapotevu.
Unajifanya mzungu, kiswahili si sikivu.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Si uturi si udwanzi, bali ni tele jalala.
Mungwa muelezi, udumu kumcha mola.
Sio yule mpuuzi, udumisha takabula.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli thadhari.

Ninamuomba rabuka, atutoe takabuli.
Atupe roho hakika, zenye mawazo mazuli.
Na sio zo kurupuka, zopungukiwa akili.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Hapa ndipo mwisho wake, ashiri beti zatosha.
Nilowapa myashike, wengine kuelimisha.
Moyoni na yawafike, lo ghafuri kukumbusha.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Bilali Kaluta

BABA

Moyoni tuna majonzi,kutokwa na wetu baba
Haya yote ni mapenzi, Ya Mola wetu Tawaba
Hakika tutakuenzi, Daima kwa zetu huba
Rabi mrehemu Baba, Muweka pema Peponi

Ulikua ni mzuri, sura na mweupe pia
Ucheshi na uhodari, pale unapo ongea
Haukua na kiburi, Mola alikuongoa
Rabi mrehemu Baba, Muweka pema Peponi

Ulipenda mahubiri, ujumbe kuuzagaza
Wamasihi wa bashiri, Ahmadi wa Mirza
Wala huku fanya siri, jamati kuitangaza
Rabi mrehemevu Baba, Muweka pema Peponi

Kazi ilikua nzito, ujumbe kuusambaza
Amani na magoroto, Gombero pia muheza
Lusanga hadi Lushoto, Kote huko hukusaza
Rabi mrehemevu Baba, Muweka pema Peponi

Ulishika uraisi, jamati tanga mjini
Mengi uliya asisi, Masijidi ihsani
Pamoja na bin habsi, Abdallah wa Omani
Rabi mrehemu Baba, Muweka pema Peponi

Ulifanya kubwa kazi,wana wako kuwalea
Ukimuomba Azizi, Dini kuwaongokea
Dunia hukuienzi,Akhera ulipambia
Rabi mrehemu baba, Muweka pema Peponi

Tunakuomba Mwenyezi, Mola wetu wa Rabuka
Abasi apande ngazi, Moto aweze epuka
Nasi wanawe wapenzi,mema yake kuyashika
Rabi mrehemu Baba, Muweka pema Peponi

Leo ninaweka wazi, siku ulipo jifia
Wanajamati wapenzi, Dua walikuombea
Naye swalehe wa pazi, Daima takuombea
Rabi mrehemu Baba, Muweka pema Peponi

Tamati ninafikia, Baba ninakukumbuka
Tudumu kumuombea, yeye pamwe na kizuka
Buriani tangulia, zamu yetu itafika
Rabi mrehemu Baba, Muweka pema Peponi

Rajabu Abasi Mkieti
AL-WATTANI MLEZI
Lusanga Muheza Tanga

ALLAHU AKBAR

Juma mosi ile yeye hawezi kuisahau, huyub ni kijana mdogo aitwaye Abdullah yaani 'mtumishi wa Allah' anayeishi katika kata ya azimio wilayani ubungo.

Aliishi na wazazi wa kambo ambao walimuokota kutoka dampo la tabata. Wazazi hawa japo walikuwa na ubinadam, lakini pombe, madawa, uongo, visasi, mauaji ilikuwa ni sehemu ya maisha yao. Wao wanasema "hivi vyote tuvifanyavyo ni mipango ya Mungu"

Uongo wao ulimfanya Abdullah kutokuwa na imani kwa mungu hata kidogo. Baada ya kuambiwa hata wazazi wake walifariki kwa ajali "huo pia ni mpango wa mungu" wao walisema.

Abdullah alikataan kuitwa jina lake na kujiita SIMTAKI MUNGU. Yeye alifanya matendo maovu, mabaya na ya kustaajabisha wilayani mule. Yote kwa yote simtaki mungu alipenda sana masomo yake, ijapokuwa kila mtihani alioufanya jumamosi alipata chini ya 2%.



Siku moja alipokua anelekea shuleni, alimuona bibi kizee mmoja akiangaika kubeba kuni zake, roho ya huruma ilimpata na kumsaidia bibi yule hadi karibu na shule yao. Bibib yule alimshukuru sana simtaki mungu.

Baada ya masaa 10 kupita matokeo yalifika, lakini cha kushangaza hakuliona jina lake katika karatasi, alimuuliza mwalimu wapi jina langu? Mwalimu alikua amebanika sana hivyo hakumjibu.

Punde rafiki zake walifika na kumtaarifu kuwa amefanyaje mpaka amepata alama 60% kwa mtihani ule. Aligutuka na kwenda tena katika karatasi. Kumbe jina lake leo halikuwa chini bali katikati ya karatasi.

Simtaki mungu alifurahi sana kuliko siku zote za masiha yake. Akiwa anarejea na tabasamu pana alimuona bibi kizee akikoleza moto. Hapo aligundua itakuwa ni sababu ya msaada aliotoa hapo akanong'ona kimoyo moyo na kusema "kumbe mungu si mbaya sana ee"

Sikju ya ijumaa kabla ya jumamosi ya wiki niliyofuata, simtaki mungu aliimgia msikitini pia akatoa sadaka na kumhimili sana Allah.

Safari hii kwenye mtihani hakuwa amepata 60% tena bali 99%. Maendeleo yake yalimshangaza kila mtu, wanafunzi wenzake, walimu majirani na hata wazazi wake. Walipomuuliza yeye alibaki tu kusema Allahu Akbar.

Hakuna tena simtaki mungu yule tuliyemjua bali yeye na Abdullah pekee.

Hadithi na Zaid A. Machombe, Mabibo - DSM

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

NIKAH	DHIAFAT	UNAJIMU	TABIBU
IKHLAS	TANBIHI	URUHUBANI	KURUNZI
IHLAM	ZIRAAT	ISLAMABAD	HADUBINI
KHILAFAT	KIKOKOTOZI	MARKAZ	DARUBINI
MAHDI	TAWHIID	MULAQAT	ISTIGHFAR
WAQFEEN	TANZIA	MUADHAM	
UTANDAWAZI	MDAHALO	MHANDISI	
TADHKIRAH	UPAGANI	MAULANA	

J	Z	I	Z	Z	T	L	J	I	N	A	G	A	P	U	I	C	P	T
T	X	N	K	P	T	T	G	M	H	R	T	G	V	N	Z	I	C	J
B	I	I	J	M	M	C	N	N	A	H	N	A	I	M	H	N	L	N
R	S	B	U	A	Z	B	Q	R	K	J	A	B	W	I	N	L	Q	N
G	T	U	M	H	T	T	R	G	I	V	U	R	B	H	W	M	M	M
T	I	D	I	D	A	N	R	Y	N	R	L	N	I	Y	I	A	C	U
A	G	A	J	I	F	I	H	L	A	M	A	M	C	K	U	I	H	L
N	H	H	A	M	A	R	Z	D	K	T	U	M	A	L	H	R	D	A
Z	F	X	N	L	I	M	T	O	T	H	D	B	A	R	I	D	L	Q
I	A	C	U	X	H	N	M	W	T	A	I	N	I	N	K	G	A	A
A	R	B	J	L	D	M	T	T	H	O	A	L	A	B	W	A	D	T
Z	I	Z	A	W	A	D	N	A	T	U	K	B	A	A	A	P	Z	M
M	W	M	N	L	B	N	L	V	N	T	U	O	Q	F	N	T	U	I
T	F	V	L	H	L	O	M	F	R	H	S	F	K	N	A	A	B	Z
D	P	Z	I	R	A	A	T	K	U	A	E	J	X	I	D	T	B	N
I	S	I	D	N	A	H	M	R	L	E	Q	P	B	H	K	M	N	U
X	N	M	T	N	N	T	U	H	N	P	N	M	A	T	L	L	Z	R
K	C	M	R	N	H	F	K	X	V	C	R	M	P	N	Q	H	P	U
K	T	R	X	K	X	I	S	L	A	M	A	B	A	D	V	Y	F	K

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jabali la Mahubiri Limetutoka!

Kutoka uk. 3

Mwalimu kwani akimaliza masomo hayo atachagua sasa dini ipi na dhehebu gani ni la kufuata.

AANZA MASOMO KWA SHEIKH WA JUMUIYA YA AHMADIYYA

Mwanafunzi Abasi Mkieti kila siku alikuwa akija muda mchache kabla ya sala ya Maghrib. Hapo atamkuta maulana Sheikh Abuutwalibu amesha fika na amesha jiandaa kwa kila somo alilolitaka mwanafunzi wake. Baada ya masomo kulifata kipindi cha maswali cha mwanafunzi kwa mwalimu kwa kawaida huja na maswali yasiopungua 10 yote Sheikh alikua akiya jibu siku zilivyozidi kwenda maswali yalizidi kupungua hadi kubaki hana swali hata moja.

Kitu hiki kilimvutia sana kwani katika dini zote na makundi yote alikopita, badala ya maswali kupungua yalikuwa yanazidi hapo ikizidi kumtia mashaka na kuona katika dini hizo sio sahihi.

Sheikh alikidhi kiu ya Mwanafunzi hapo alilazimika Mwalimu kumuuliza maswali mwanafunzi kila siku darasa halikufa kwani kila siku kuna somo jipya.

Katika masomo yake, somo la uungu wa Yesu Kristo lilikuwa ni la kumtatiza sana kwani katika madhehebu hayo ya dini ya Kikristo hayakumuafiki kukubali kwani yeye alikuwa akiwauliza juu ya ibada ya masanamu na kinachowekwa mbele kwenye ibada za Kikristo jambo hilo aliweza kulielewa vizuri zaidi baada ya kupata ufafanuzi wa Sheikh Abutwalibu Sandi. Aliendelea na masomo huku akiwa hajaacha kwenda kwa father wa kanisani.

Siku moja father alikuja kwa mwanafunzi wake katika sehemu anayofanyia kazi kama kawaida yake akakuta kuna mazungumzo yanayo husu juu ya uumbaji wa ndege wa Yesu Kristo. Bwana Abasi Mkieti aliulizwa na bwana mmoja juu ya jambo hili yeye hakupenda kujibu kutokana na ujio wa Mwalimu wake ila yule mtu ambaye alikua anamuuliza aliendelea kusisitiza swali lake bwana Abasi Mkieti akaona hakuna njia ila ni kujibu sawa na elimu alionayo maelezo aliyo yatoa yalikua ni mapana mno kwani kwa wakati huo yule Mwalimu alikua amejinyamazia. Father aliporudi kanisani alimuita sister na kumueleza kuwa yule mwanafunzi unayemfundisha kuanzia leo usimfundishe kwani yeye ni Mwalimu kama mimi na sio mwanafunzi. Bwana Abasi Mkieti alipofika sister akamwambia nimeambia nisikufundishe kuanzia leo yeye 'father' Padre atakuwa anakufundisha mwenyewe kwani wewe ni Mwalimu kama yeye. Kuanzia hapo ndipo alipokuwa anafundishwa na father Odilo hadi alipoamua kuacha na kuendelea kusoma katika msikitini wa Ahmadiyya Tanga.

SHEIKH ISMAIL MUNIR AFIKA TANGA

Hapo alikuwa zama mpya za elimu ya Mzee Abasi Mngodo Mkieti kwani Maulana akaanza kufundisha Yassarnal Qu'ran na katika kipindi hicho ndio akiwa tayari ameshajiunga na jamaat Ahmadiyya kabla ya Sheikh Abutwalibu kuhamishwa.

Pia akasoma Quran Tukufu na soma la Biblia lilimjenga kuwa Mhubiri na kufanya kuaminika sana hata katika mihadhara mbalimbali akipangwa sehemu yoyote alikuwa tayari kutekeleza.

Mzee aliweza kupita maeneo mbalimbali ya mkoa wa Tanga akiwa na wazee mbalimbali kama Hashim Chuma, Mzee Maulidi Kaguta, Mkuu Chuo, Mzee Abdallah Salimu Seifu wa Oman.

Mzee Abasi Mkieti pamoja na wanajamati kama kina Mzee Maulidi Kaguta, Hashim Chuma, Abdallah Salimu wa Oman Wengine waliweza kupita maeneo mbalimbali ya mkoa wa Tanga wakifanya Mahubiri kwa pesa zao.

Mzee Abasi Mkieti alikua Raisi wa jamaat ya Tanga mjini kwa kipindi cha muda mrefu mpaka mwaka 2007.

Katika kipindi cha enzi za nyuma aliweza kushiriki na Masheikh na walimu mbalimbali katika kazi ya mahubiri kama Maulana Sheikh Ismail Munir, Sheikh Bakri Kaluta, Sheikh Tahir Khan, Mwl Athuman Mgunya, Mwl Maliki Mbawala.

MARADHI HADI KIFO CHAKE.

Mwezi Novemba 2018 afya ya Mzee Abasi Mkieti ilianza kudhofika kwa ugonjwa wa shinikizo la damu. Tangia kipindi hicho wataalamu waliendelea kumpatia matibabu ikaonekana ni lazima kufanyiwa upasuaji. Mwaka huu 2019 mwezi 5 upasuaji ulifanyika na tangu hapo afya yake haikutengemaa tena. Maulana Sheikh Muhammad Afzal Bhatt wa Tanga aliwaomba wanajamati siku chache kabla ya kifo cha Mzee Abasi kufanya maombi maalumu katika siku ya Ijumaa katika maombi hayo inasemekana watu wengi walitokwa na machozi na vilio vya kwikwi wakati maombi yanaendelea. Mnamo tarehe 1/06/2019 saa 4:00 asubuhi katika hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Tanga Bombo Mzee Abasi Mngodo Mkieti aliaga dunia. ***Innalillah Wainna Ilaihi Rajiun.***

Salamu za pole zilimiminika toka ndani na nje ya nchi zikiongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu Maulana Shekh Tahir Mahmood Chaudhry sahib kwa familia kwa kupoteza askari mahiri katika uwanja wa Mahubiri. Siku ya 2/06/2019 majiri ya saa 8:00 mchana mwili wa askari huyu wa Masihi Aliyeahidiwaas ulifika katika kijiji alichozaliwa Lusanga Muheza na kuzikwa. Mazishi yalihudhuriwa na wanajumuiya kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania.

Nalia mie nalia,
Machozi yangu sikia,
Naomba wangu Jalia,
Akae palotulia,
Firdaus Nuzula

Mhariri

Bi Fatma Bakari Mbihila Katangulia



Na

Abdallah

Msesemele

Mwaka 1990, Bwana Amran Duage wa Kiteto alijaaliwa kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya. Ilikuwa ni msaada wa Allah ulioptia katika jitihada zake kubwa za kusoma vitabu vya Jamaat. Kila hoja alizozipata katika vitabu hivyo aliwauliza Masheikh ambao hawakuwa na jibu la kuridhisha, hivyo mwaka huo wa 1990 akajiunga na Ahmadiyya.

Hapo ndipo tunapopata maana hasa ya kuzaliwa mara ya pili. Ibada ziliongezeka, huruma na wem, vyote hivi vikaleta mabadiliko makubwa pale nyumbani kwake. Lakini mke wake siku nyingi kabla alikuwa ameshaa acha kwenda msikitini, kama alivyodai kutokana na maneno maneno yasiyo na uhusiano na nyumba ya Allah. Hatimaye kutoka Arusha walihamia Tanga na pale tuna msikiti na Bwana Amrani Duage akamuomba mkewe ambaye alikuwa bado hajajiunga na Jumuiya aende msikiti wa Ahmadiyya. Bi Fatma alikubali, lakini na hofu ile ile ya misikiti aliyokuwa nayo akawa anakaa pembeni lakini akina mama wa Kiahmadiyya kana kwamba wanamfahamu kwa siku nyingi walimkaribisha kwa furaha na bashasha na kwa mara ya kwanza akasikia ladha ya kuwa msikitini. Utulivu mkubwa ulipatikana mpaka akawa haamini kilichokuwa kinaendelea. Mazungumzo ya akina mama, mapenzi waliyomuonesha, hakuwa na njia isipokuwa kujiunga na Ahmadiyya. Mabadiliko makubwa kwake yalitokea lakini haya yalikuwa ni mwiba katika familia yake. Baba yake mzazi ambaye alikuwa ni Sheikh hakufurahishwa na jambo hilo na alifanya kila njia atoke katika Jamaat. Lakini Bi Fatma alisimama imara kama nyota ya zuhura. Hata hivyo baba yake aliendelea kutoa vitisho lakini mbinu zote hizo hazikufua dafu. Bwana Amrani Duage alifariki, *Innalillah Wainna Ilaihi Rajiuun*, na kumuacha Bi Fatma akiwa na watoto watano na baba mzazi akaona sasa ni nafasi nzuri ya kumtoa binti yake katika shimo la upotofu. Lakini Bi Fatma aliendelea kuwa imara na akiwaimarisha pia mabinti zake, huu ni ujasiri na mfano wa kuigwa. Mipango ya Allah ni mikubwa. Marehemu Mwalimu Mohammed Sudi Namwete alipelekwa Dodoma na moja ya sehemu ambazo zilikuwa chini yake ilikuwa ni Kiteto. Akiwa huko aliweza kukutana na Bi Fatma na wakafunga ndoa. Yalikuwa ni Maisha ya furaha na Maisha ambayo yalitoa mfano mzuri kwa wana tawi waliokuwa chini ya Mwalimu Namwete. Bila shaka kazi nzuri aliyoifanya Mwalimu Namwete katika mahubiri na malezi nyuma yake palikuwa na msaada mkubwa wa Bi Fatma. Na huu ndiyo ukweli wa Maisha ya kwamba mafanikio yote ya wanaume nyuma ya pazia bila ya kutoa sauti kuna msaada mkubwa wa mwanamke. Bi Fatma alijitahidi sana katika kufuata mafundisho ya Jamaat Ahmadiyya na siku alipokutwa na mauti alikuwa anatizama MTA. Nadhani hakuna somo zaidi alilotuachia ni hilo la ***kuenzi na kuheshimu kazi kubwa inayofanya na MTA*** ambayo kwa hivi sasa ndiyo ***Chuo Kikuu cha elimu ya Islam duniani***.

MATUKIO KATIKA PICHA



Idi ul Adh'ha Jamia Morogoro



Idi ul Adh'ha Iringa



Idi ul Adh'ha Kahama



Maonyesho ya Nanenane Tabora



Idi ul Adh'ha Tanga



Idi ul Adh'ha Zanzibar



Maonyesho ya Nanenane Ruvuma



Maonyesho ya Nanenane Bukoba



Maonyesho ya Nanenane Zanzibar



Maonyesho ya Nanenane Arusha



Maonyesho ya Nanenane Dodoma



Maonyesho ya Nanenane Mbeya



Maonyesho ya Nanenane Mtwara na Lindi



Maonyesho ya Nanenane Mtwara na Lindi



Wanafunzi wa Jamia Ahmadiyya wakitazama Jalsa Salana Uingereza 2019 kupitia MTA Africa



Wanajamaat wa Morogoro wakijitolea damu kwa wahanga wa ajali ya moto iliyotokea Msamvu baada ya Lori la mafuta kulipuka na kuleta maafa makubwa

Darasa La Qur'an Tukufu

UMUHIMU WA CHAKULA KATIKA MWILI WA MWANADAMU

Enyi watu! kuleni katika vile vilivyomo ardhini, vilivyo halali na vyenye kufaa kiafya, wala msifuate nyayo za Shetani; bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri. (Surah Al-Baqarah : 169)

Vilivyo halali na vyenye kufaa kiafya. Ni wazi kuwa chakula huleta athari juu ya kiwiliwili cha mtu na juu ya roho yake pia. Chakula kisicho halali huharibu imani ya mtu, maana ni kunyume cha amri ya Mwumbaji wake. Na chakula ambacho si kizuri hudhuru kiwiliwili chake. Basi, ilikuwa lazima kwa dini iliyo kamili kueleza habari kamili katika jambo hili. Islam inasema:

1. Chakula kiwe halali, yaani kilichoruhusiwa na sheria ya Allah.
2. Kiwe kizuri kinachofaa kiwiliwili cha binadamu. Maana mwenye kiwiliwili kibaya na roho najisi hawezi kutimiza kusudi la kuumbwa kwake.

Neno TWAYYIB linaweza kutumika katika uchaguzi wa mtu binafsi na pia hali ya uzuri kiafya wa kile kitu ambacho kimetangazwa kuwa halali. Katika maana ya kwanza chakula kile kile ambacho ni halali chaweza kuwa twayyib kwa mtu mmoja na kikawa siyo TWAYYIB kwa watu wengine kutokana na kuhitilafiana katika uchaguzi, muonjo na mazingira.

Katika maana ya pili neno TWAYYIB laweza kuirejea ile hali ya chakula likiashiria kwamba waaminio wanapendelea kula chakula ambacho siyo tu ni halali bali pia chapatikana katika hali nzuri, ya uzima na ya kiafya.

UMUHIMU WA CHAKULA

Chakula ndio hutumika kuzalisha na kulisha chakula kwenye seli. Chakula hutumika kukinga na kutibu magonjwa. Chakula husaidia kuweka nguvu ya mwili (energy). Chakula husababisha virutubisho mbalimbali vya mwili n.K

MADHARA YA CHAKULA

1. Tabia - Tabia ni Matokeo ya Mawazo (UBONGO) na HISIA (MOYO). Mifumo ya Ubongo na Moyo Ufanyaji kazi kadri ulivyo kadiriwa hutegemea Chakula cha aina gani. Maana chakula ndio kinacho jenga mwili. Ni sawa na aina ya matofali ya Udongo aina fulani basi nyumba huonekana katika sura ile ya udongo.

Chakula Vipo Vyenye tabia mbalimbali. Ukali, Upole, Huruma, Ukatili, wivu, n.k.

Hivyo basi Allah Alihitaji mufumo fulani ili kujenga TABIA NJEMA. Chakula hivyo Vitaitwa HALALI na TWAYYIB (Kizuri na chenye kufaa)

Wanasayansi wamekiri kuwa chakula kina uhusiano wa moja kwa moja na tabia za mwanadamu.

2. Chakula husababisha Wema na Taqwa (18:20). Tabia ya huruma, kusamehe, ukali, subira, ukweli hutengenezwa na mifumo ya chakula. Allah Akahalalisha baadhi ya chakula na kufanya twayyib baadhi ya chakula kwa kusudio hili. Mfano ulaji wa nguruwe kuna kufanya kubeba tabia ya nguruwe ya uzinifu, kufanya uovu bila haya n.K hivyo kuacha kula nguruwe ni msaada kwa mwanadamu asikurubie maovu hayo. Unywaji wa ulevi humharibu mwanadamu hivyo kuacha ni msaada kwa mwanadamu.

3. Chakula ni Tiba ya Magonjwa mbalimbali na Afya katika mwili wa Mwanadamu. Magonjwa ya Moyo, Kisukari, Magonjwa ya Ngozi, Cancer, n.k Mengi yao hutokana na Chakula ambacho sio HALAL NA TWAYYIB. Tangawizi ni Tiba ya magonjwa mbalimbali, Chakula kina carbohydrates, Protein, Vitamin ambazo hutumika Kujenga Mwili na Afya na tiba kwa Mwanadamu. Wakati huo huo Chakula husababisha Magonjwa kikiwa sio Halali na Twayyib au Kuzidi (kupungua au kuzidi).

MAHITAJI YA CHAKULA

Mwili huhitaji wanga (Carbohydrates), Vitamini (13 ikijumuishwa A, B, C, D, E na K), Mafuta (Fat), Madini kama Kalshiam (Calcium), Magnezi, Protini, (Nyuzinyuzi Fibres na MAJI

Chakula Halali na Twayyib ni kile kinachotoa kiwango kinachohitajika mwilini.

Chakula kiliwe kwa Kipimo sawa na haja ya Mwili.

Hivyo kwa manufaa ya mwili Allah Alihitaji tu vyakula fulani ndio viliwe kufanya mwili ustawi kwa afya yake. Vinginevyo ni kuenda kinyume chake na Kujisababishia madhara.

Huhitaji kuainishwa kila chakula ila chunguza kila chakula kilichokatazwa utaona madhara yake kwenye mwili wa mwanadamu.

Imeandaliwa na **Musa Salum** 0717 504 690

Allah Atujaalie tuwe wenye kula vyakula ***HALALI*** na ***TWAYYIB***. Amin

Madhumuni ya Jalsa Salana

Imefasiriwa na Ahmad Abdulrahim

Duniani hufanyika mikutano mingi ya aina tele, ambapo watu hukusanyika kwa sababu tofauti tofauti. Mikutano hii hutofautiana kutokea ya kisiasa, matamasha ya miziki, matukio ya michezo na kila kitu kati ya hayo. Watu hunufaika kwa namna mbalimbali kutokana nayo, iwe kwa burudani tu, faida za kiafya au kuimarisha nafasi zao za kisiasa.

Hata hivyo, mikutano si kwa faida za kidunia tu. Hija ni mfano wa msingi wa hili. Malipo ya kiroho na faida anazoweza kuzipata mtu kutokana na kuhiji huku huweza kuwa mbali na ufahamu wa kibinaadamu.

Mkusanyiko mwingineo ni Mkutano wa Mwaka wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya (Jalsa Salana). Ilipoanzia kiunyonge 1891, katika kijiji cha mbali cha Qadian, ambapo ulihudhuriwa na wanachama 75 tu hivi wa Jumuiya, imepanuka maridhawa sasa. Mikutano hii inafanywa katika nchi mamia katika ngazi ya kimataifa, wakati mwingine ikiwa na washiriki zaidi ya 39,000 kutoka mamia ya nchi.

Kuna zaidi katika mkutano wa mwaka kuliko yayaonayo macho. Mkutano huu uliasisiwa na mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya, Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as}. Yeye (amani iwe juu yake) aliainisha madhumuni makuu manne ya mkutano huu:

1. Kuongeza ukaribu wa mtu na Mungu Mwenye Jalali.
2. Kuwaombea wale ndugu waliofariki.
3. Kukutana na wanachama wapya na kuongezeka undugu.
4. Kupata na kujiongeza katika elimu.

Malengo haya manne ya msingi yaliyowekwa na Masihi Aliyeahidiwa^{as} yanatimizwa katika kila nyanja ya Mkutano wa Mwaka (Jalsa Salana). Kidhahiri hususan mlengo wa kuongeza maungano ya mtu na Allah Mtukuka. Pamoja nayo ratiba nzima ikizizunguuka sala tano za kila siku, mtu hujikuta katika mazingira yasiyoepukika ya kuongeza imani. Na zaidi ni pale mkutano unapobarikiwa na uwepo wa Khalifa wa zama, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad atba, kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya duniani. Kusali ala tano kila siku nyuma ya Khalifa huichochea athari ya mtu ya kiroho.

Mwisho, mtu anaweza kutimiza lengo la kupata elimu kwa kusikiliza hotuba za Hadhrat Mirza Masroor Ahmad atba, kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya duniani ambazo huwa dafina ya mafundisho asili ya Islam na kazi ya Islam katika zama zetu. Hotuba zilizojaa elimu za wataalamu wa Jumuiya hupangwa katikati ya ratiba nazo hutoa nafasi tele kwa dhumuni hili, na pia maonyesho mbalimbali yanayowekwa na idara tofauti tofauti.

Hivyo, inapaswa kukumbuka madhumuni halisi ya mikutano ya mwaka (Jalsa Salana) tunapoihudhuria yaliyowekwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s., kwa sababu faida ya kiroho na manufaa ndiyo yanayoitofautisha mikusanyiko mingine ya kidunia na mkutano huu.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA

TUMBAKU

"HATUWEZI kuihesabu tumbaku miongoni mwa vilevyavyo, lakini kwa vyovyote ni kitu cha kipuuzi. Na sifa ya waaminio ni kwamba 'wanajiepusha na vitu vya kipuuzi'.nKama mtu fulani ameambiwa na daktari kuvuta tumbaku Kama tiba, hatumkatazi. Lakini kwa jumla hicho ni kitendo kisicho na maana tena ni kuharibu Mali bila sababu. Kama tumbaku ingekuwa katika zama za Mtume^{saw}, bila shaka yeye naye angeichukia" (Al Hakam 22.3.1903).

"Kuhusu tumbaku ni kwamba ingawa hiyo siyo Kama ulevi hata kwamba imwelekeze mtu kwenye uovu, lakini hata hivyo ucha-Mungu ni kuepukana nayo. Kinywa kinanuka kwa sababu ya kuvuta tumbaku. Tena ni sura ya kuchukiza kuvuta moshi ndani na kisha kuutoa."(Al-Badr 3.4.1903).

Kuhusu tumbaku, sheria haikusema, lakini tunaihesabu kati ya 'makruhi' (kinachochukiza), kwani Kama ingelikuwa katika zama za Mtume^{saw}, yeye angelikataza kuivuta". (Al-Badr 24 Julai 1903).

Hadhrat Zaid Bin Harith ra

Inatoka uk 12

anavaa mavazi marefu na kufuga nywele ndefu. Kuna hadithi moja katika kitabu cha Mustadrak Al-Hakim kuwa Hazrat Khuraim ra bin Fatik anasimulia kwamba safari moja Mtukufu Mtume saw alisema: "Ewe Khuraim! Ungekuwa mtu bora ikiwa unaacha mambo haya mawili ambayo ni kufuga nywele ndefu na kuacha mavazi yako yaburuzike chini ya miguu". Hivyo mara moja akayaacha mambo hayo kutokana na maagizo ya Mtume Mtukufu saw. Kwa ajili ya wanaume urefu wa nywele unatakiwa kufika hadi ndewe tu na hawatakiwi kufuga nywele ndefu kama wanawake bila kuwa na sababu maalum.

Sahaba mwingine ni Hazrat Ma'mar bin Harith ra alitokana na kabila la Banu Jumu'ah la Quraish. Alikuwa na kaka wawili - Hatib na Hattab. Wote watatu walikuwa miongoni mwa waliojiunga na Uislamu mwanzoni hata kabla Mtume Mtukufu saw hajahamia Dar-e-Arqam. Mtukufu Mtume saw alifunga udugu kati ya

Hazrat Ma'mar ra na Hazrat Mu'adh bin Afraa. Hazrat Ma'mar ra bin Harith alishiriki katika Vita vya Badr, Uhud, Khandak na vita vingine vyote pamoja na Mtukufu Mtume saw. Hazrat Ma'mar bin Harith ra alifariki dunia mwaka 23 Hijria katika enzi ya Ukhalifa wa Hazrat Umar ra. Sahaba anayefuata ni Zuhair bin Raafi ra. Alikuwa kaka yake Hazrat Muzahir ra aliyetajwa hapo juu. Hazrat Zuhair ra alitokana na tawi la Banu Haritha bin Harith miongoni mwa makabila ya Maansar. Hazrat Zuhair ra alikuwepo wakati wa Baiat ya Pili ya Aqabah na alishiriki katika Vita vyote pamoja na Mtukufu Mtume saw. Sahaba mwingine ni Hazrat Amr bin Iyaas ra. Alitoka Yemen na aliungana kwa mapatano na kabila la Maansar liitwalo Banu Lauzan. Hazrat Amr alishiriki katika Vita vya Badr na Uhud pamoja na Mtukufu Mtume saw. Hazrat Amr ra alikuwa kaka yake Hazrat Rabi' bin Iyaas na Hazrat Warqah bin Iyaas ra ambao wote watatu walipata nafasi ya kushiriki Vita vya Badr. Sahaba mwingine ni Hazrat Mudlij bin Amr ra. Jina lake pia linajulikana kama Midlaaj katika vitabu vya Hadithi. Alitokana na tawi la Banu Hajar la kabila la Banu Sulaim na walikuwa wasaidizi wa kabila la Banu Kabir bin Ghanam bin Dudaan. Hazrat Mudlij ra alishiriki katika Vita vya Badr pamoja na kaka zake wawili, Hazrat Saqaf bin Amr ra na Hazrat Malik bin Amr ra. Hazrat Mudlij bin Amr ra alishiriki katika Vita vya Badri na vingine vyote pamoja na Mtume Mtukufu saw. Alifariki mnamo 50 AH wakati wa utawala wa Hazrat Amir Mu'awiyyah. Sahaba mwingine ni Hazrat Abdullah bin Suhail ra. Hazrat Abdullah pia alijulikana kwa jina Abu Suhail na alitokana na kabila la Quraish liitwalo Banu Aamir bin Loi. Mwanahistoria Ibn-e-Ishaaq amemtaja Hazrat Abdullah bin Suhail katika kitabu chake kuhusu historia ya Kiislamu katika masimulizi ya Hijra ya kwenda Uhabeshi mara ya pili. Wakati Hazrat Abdullah bin Suhail aliporudi kutoka Uhabeshi, baba yake alimfunga na akamlazimisha kuacha dini yake. Kutokana na mateso makubwa Hazrat Abdullah ra bin Suhail alikubali kwamba atajitoa katika Uislamu na katika Vita vya Badri akaenda pamoja na jeshi la makafiri. Wakati majeshi yote mawili yalikuwa yanatazamana, Hazrat Abdullah bin Suhail alitoka humo na akaja kujiunga na jeshi la Waislamu. Hivyo, alipigana Vita vya Badr upande wa Waislamu. Baada ya ushindi wa Makka, baba yake Suhail bin Amr alitangaziwa kupewa ruhusa maalum kutoka kwa Mtume Mtukufu saw. Mtume Mtukufu saw alisema Suhail bin Amr kwa kweli ni mtu mzuri na mwenye akili sana. Anazo sifa njema zitakazomsaidia na atajiunga na Uislamu. "Hazrat Abdullah ra bin Suhail alimhadithia baba yake kauli ya Mtume Mtukufu saw naye akajibu:" Ninaapa kwa Mungu! Muhammad saw alikuwa mwadilifu katika ujana wake na hata katika uzee wake." Katika siku za baadaye kutokana na mwenendo mzuri wa Mtume Mtukufu saw Suhail pia aliongoka na alikubali Uislamu.

Sahaba mwingine ambaye nitamtaja ni Hazrat Yazid bin Harith ra, ambaye alitokana na

ukoo wa Banu Ahmar bin Haritha wa kabila la Ansar la Khazraj. Jina la baba yake lilikuwa Harith bin Qais na jina la mama yake lilikuwa Fusham. Hazrat Yazid pia alijulikana kama Yazid Fusham na Yazid bin Fusham kutokana na mama yake. Mmoja wa kaka yake alikuwa Abdullah bin Fusham.

Baada ya kuhamia Madina, Mtume Mtukufu saw alifunga udugu kati ya Hazrat Umair na Hazrat Yazid bin Harith. Nao wote wawili walibahatika kushiriki katika vita vya Badr na wakauawa shahidi.

Sahaba mwingine atakayetajwa ni Hazrat Umair bin Humaam ra aliyetokana na tawi la kabila la Khazraj la Maansar liitwalo Banu Haraam bin Ka'ab. Wakati wa kuhamia Madina, Mtukufu Mtume saw alifunga udugu kati ya Hazrat Umair bin Humaam na Hazrat Ubaidah bin Harith Muttalbi. Masahaba wote wawili walikuwa miongoni mwa wale waliouawa shahidi katika vita vya Badri. Wakati wa Vita vya Badr, makafiri walipokuwa wanakaribia, Mtume Mtukufu saw alisema: "Songeni mbele kupata Pepo ya Allah ambayo upana wake umeenea hadi mbinguni na ardhini." Hazrat Umair bin Humaam aliuliza: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Ulisema kwamba Pepo imeenea hadi mbinguni na ardhini? Mtume Mtukufu saw akajibu, "Naam". Naye akasema, "Bakhe Bakhe [ni maneno ya kuonesha mshangao na furaha]." Hivyo Hazrat Umair ra bin Humaam alianza kupigana vita na makafiri na mwishowe akauawa shahidi.

Sahaba mwingine ni Hazrat Humaid ra Ansari. Hazrat Zubair ra anasimulia kwamba safari moja alikuwa anabishana kuhusu maji ya umwagiliaji na Ansar mmoja aliyewahi kushiriki katika vita vya Badr. Ili kumaliza mabishano wakapeleka kesi yao kwa Mtume Mtukufu saw kwa sababu wote wawili walitumia njia hii ya maji kumwagilia ardhi. Mtume Mtukufu saw akamwambia Hazrat Zubair ra, "Zubair, unapaswa kumwagilia ardhi yako kwanza (kwani ilikuwa ni ardhi yake) kisha uwaachie maji jirani zako. Baada ya kusikia uamuzi huu, yule mwenzake Ansari alikasirika na akasema, "Ewe Mtume wa Allah s.a.w., je! Umemruhusu kwa sababu yeye ni binamu yako?" Rangi ya uso wa Mtume Mtukufu (saw) ilibadilika na kuwa nyekundu kwa maana hakulipenda jambo hilo na akamwambia Hazrat Zubair ra, "Nilikushauri kuwa umruhusu mwenzako pia kutumia maji kama hisani lakini sasa ni suala la haki ya mtu. Kwa hiyo una haki ya kutumia maji mpaka yarutubishe ardhi yako na unaweza kabisa kuyazuia kutokana na mienendo ya mwenzako." Urwah anasema kwamba Hazrat Zubair ra alikuwa anasema, Nafikiri aya ifuatayo ilishuka kutokana na tukio hilo kuwa,

La, Ninaapa kwa Mola wako! Hawataamini mpaka wakufanye wewe kuwa hakimu katika wanayohitilafiana kwayo, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu unayotoa nao wanyenyekee kabisa. (4:66)

Katika vitabu vya Al-Asaba, Usdul Ghaba na maelezo ya Sahih Bukhari jina la Ansar huyo pia limetajwa ambaye alihitilafiana na Hazrat Zubair ra. Alikuwa Hazrat Humaid Ansari ra, ambaye alishiriki katika vita vya Badr lakini pengine yawezekana kabisa kuwa shetani kuwashawishi watu kisirisiri. Kwa vyovyote, Allah Ametangaza msamaha Wake kwa wale wote walioshiriki katika Vita vya Badr. Sahaba mwingine ni Hazrat Amr bin Muaz bin Athir ra. Mtukufu Mtume saw alifunga udugu kati ya Hazrat Amr bin Muaz ra aliyekuwa miongoni mwa Maansar na Hazrat Umair bin Abu Waqas ra ambaye alihamia Madina kutoka Makka. Umair bin Abu Waqas alikuwa kaka yake Hazrat Sa'd bin Abu Waqas. Hazrat Amr ra bin Muaz alishiriki katika vita vya Badr pamoja na kaka yake, Hazrat Sa'd ra. Hazrat Amr bin Muaz ra aliuawa shahidi katika Vita vya Uhud alipokuwa na umri wa miaka 32. Sahaba mwingine ni Hazrat Masud bin Rabieya bin Amr ra. Alitokana na kabila la Qaara ambalo liliungana kwa mapatano na kabila la Banu Zuhra. Mtume Mtukufu saw alifunga udugu kati ya Hazrat Masud bin Rabieya ra na Hazrat Ubaid bin Taiyhaan ra. Hazrat Masud bin Rabieya ra alishiriki katika Vita vya Badr, Uhud na vita vingine vyote pamoja na Mtume Mtukufu saw. Hazrat Masud ra aliaga dunia mnamo mwaka wa 30 wa Hijra akiwa na umri wa miaka 60. Mungu Mwenyezi Anyanyue daraja za masahaba hawa nasi pia tuendeleze matendo yao mema. Ningependa sasa kueleza kwa ufupi kuwa InshAllah, Jalsa Salana ya Uingereza inaanza Ijumaa ijayo. Tunatakiwa kumwomba Allah Atie baraka Zake zote katika Jalsa hii. Wale ambao wamepewa majukumu mbalimbali wanapaswa kujitahidi kuyatimiza kwa bidii na uwezo wao wote. Vilevile wanapaswa kumwomba Allah ili waweze kutimiza majukumu yao kwa namna iliyo bora. Mungu Mwenyezi Awajaalie kuwatumikia wageni wa Masihi Aliyeahidiwa as vizuri. Mwaka huu kutokana na Makao Makuu kuhamia Islamabad, idara inayosimamia usafirishaji itatakiwa kufanya kazi kwa bidii zaidi kwa sababu wageni wengi watapenda kuja kusali katika Masjid Mubarak. Kwa hiyo ni lazima wajipange vizuri. Nina matumaini makubwa kuwa jambo hili watakuwa wameshaanza kulifanyia kazi. Allah Atujaalie kila mmoja wetu kutekeleza majukumu yake kwa namna inayofaa. Aamin

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

DH. QA'D - DH. HIJ 1439 AH | AGOSTI 2019 | ZAHOOR 1398 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu*saw*

Kama kila wakati mtazingatia kujiepusha na hasira basi Husuda na kinyongo vyenyewe vitatoweka. Yeyote kati yenu ashikwapo na hasira na hali amesimama, basi aketi chini, kama hasira ikiondoka kwa njia hiyo basi ni vyema waila alale chini. (Musnad Ahmad bin Hambal, J.5, uk. 152, Chapa ya Beirut).

Watu Walio Bora Kabisa
Masahaba wa Badri

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 26/07/2019; baada ya Tashahhud, Taawwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Momeneen, Mirza Masroor Ahmad*atba* alisema:

Leo, nitaendelea kutoa simulizi za maisha ya masahaba walioshiriki katika vita vya Badri. Jina la Sahaba wa kwanza atakayetajwa ni Hazrat Muzahir bin Rafay*ra*. Jina la baba yake lilikuwa Rafay bin 'Adi. Hazrat Muzahir*ra* alitokana na kabila la Banu Harithah bin Harith ambalo ni kabila mojawapo la Maansar. Hazrat Muzahir*ra* alishiriki katika Vita vya Uhud na vilevile katika vita vyote vya baadaye pamoja na Mtume Mtukufu*saw*. Hazrat Muzahir*ra* alifariki katika enzi ya Ukhalifa wa Hazrat 'Umar*ra*. Hazrat Muzahir bin Rafay Harithi*ra* aliuawa na Wayahudi na kutokana na uhalifu huo Hazrat 'Umar*ra* aliwafukuza Wayahudi wa Khaibar. Tukio la kuuawa kwa Hazrat Muzahir*ra* lilitokea katika mwaka wa ishirini baada ya Hijra. Sahaba mwingine ni Hazrat Malik bin Qudamah*ra*. Hazrat Malik alitokana na familia ya Banu Ghanam miongoni mwa kabila la Ansar liitwalo Aus. Hazrat Malik*ra* alishiriki katika Vita vya Badr pamoja na kaka yake mmoja, Hazrat Munzir*ra* bin Qudamah. Hazrat Malik*ra* pia alishiriki katika vita vya Uhud. Sahaba mwingine ni Hazrat Khuraim bin Fatik*ra* aliyetokana na kabila la Banu Asad. Hazrat Khuraim bin Fatik*ra* alishiriki katika vita vya Badr pamoja na kaka yake, Hazrat



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa kwa waaminio na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Sabrah bin Fatik*ra*. Kwa mujibu wa simulizi moja, Hazrat Khuraim*ra* alishiriki katika Mkataba wa Hudaybiyyah. Hazrat Khuraim*ra* na mtoto wake walikwenda mji wa Kufa nao wakahamia katika mji wa Raqqa, ambao ni mji maarufu unaojulikana kaskazini mwa mto wa Furaat nchini Syria. Wote wawili walienda huko katika enzi ya utawala wa Hazrat Amir Mu'awiyah. Yafuatayo ni maelezo ya Hazrat Khuraim bin Fatik*ra* anavyosimulia mwenyewe tukio lake la kujiunga na Uislamu: "Safari moja wakati wa usiku nilikwenda kutafuta ngamia wangu waliopotea nikifuata alama za njia yao. Nikawapata huko sehemu iliyoitwa Abraq-ul-Dha'f, iliyoko barabarani tukisafiri kutoka Madina hadi Basra. Niliwakuta pale, nikawafunga palepale na nikapumzika nikiegemea mguu wa ngamia mmoja. (Alikaa hapo kulala usiku kucha)."Anaendelea kusema: Asubuhi nilipoamka niliomba ulinzi kwa chifu wa sehemu hiyo kama ilivyokuwa kawaida ya wakati huo kabla ya ujio wa Uislamu. Mtu mmoja aliniita ghafla na akasema kwa ushairi: 'Mungu Akurehemu. Unapaswa kutafuta ulinzi wa Allah. Thibitisha umoja wa Mungu, na hautakuwa na wasiwasi juu ya majaribio kutoka Majinni. Dhikri ya Allah itakulinda katika nchi zote na sehemu zinazozungukwa na milima kwa maili nyingi. Njama za maadui zitashindikana na hakuna kitakachobaki isipokuwa mtu mwema na matendo mazuri.' Hazrat Khuraim*ra* akauliza: Je! Kwa kweli waamini au unanidanganya? Akajibu: Muhammad*saw* ni mtu mzuri aliyeleta aya bayana za Qur'an Tukufu zinazoeleza kila kitu. Amebainisha tofauti ya ukweli na uongo. Anatuamuru kutekeleza sala na kufunga saumu. Anawazuia watu kutenda matendo maovu na mabaya ambayo yalipatikana kati ya watu kabla yetu na hivi ndivyo tulivyopata kujifunza kuhusu ujumbe wa Umoja wa Mungu. Hazrat Khuraim*ra* akauliza, "Allah akurehemu! Wewe ni nani? "Akajibu:" Mimi ni Malik bin Malik. Mjumbe wa Allah*saw* alinituma kuangalia na kulinda Majinni ya watu wa Najjad yaani Wakuu wa watu wa Najjad. Hazrat Khuraim*ra* akajibu, "kama kuna mtu anayeweza kuchunga ngamia wangu ili niende kumwona Nabii huyo na kumkubali. Malik bin Malik akajibu: "Haina shida, nipo hapa ninawaangalia ngamia wako." Hazrat Khuraim*ra* anasema: "Nikapanda ngamia mmoja na kufunga safari ya kuelekea Madina. Nilifika wakati wa sala ya Ijumaa, kwa hiyo niliamua kusubiri nje ya msikiti mpaka wamalize sala. Abu Dhar*ra* akatoka nje na akaniambia kuwa Mtume Mtukufu*saw* anakuita ndani. Aliponiona Mjumbe wa Allah saw, alisimulia tukio lilivyotokea huko nyuma pamoja na Malik bin Malik kwa sababu tayari Allah alimwonyesha tukio hilo katika njozi. Hazrat Khuraim*ra* anasema: Kwa kusikiliza hivi nikanena, ninashuhudia kwamba hakuna aabudiwaye isipokuwa Allah na hivyo alijiunga na Uislam. Hazrat Khuraim*ra* bin Fatik alikuwa na haiba nzuri tabia ya uangalifu sana katika mambo madogo madogo. Siku zote alivaa mavazi mazuri ya kuvutia. Kabla ya kujiunga na Uislamu, alikuwa

Endelea uk. 11



JUMUIYA YA WAISLAM WAAHMADIYYA TANZANIA

inawakaribisha katika:

Mkutano wa Mwaka wa 50

Jalsa Salana Tanzania 2019

Kitonga, kata ya Msongola, Dar es salaam

0719 961 040 | 0773 546 009 | 0655 105 096

NYOTE MNAKARIBISHWA

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com